# UQAB
Jarida la



*Toleo 13 - Jamad-ul-ula 1439 AH / Februari 2018 Miladi*

**Trump na "Nchi za K**!!!"**

**Nidhamu ya Kijambazi Inayo Wapora Raia Wake**

**Siku Aliyo Lia Mtume (Rehema na Amani Zimshukie)**

**Mwanamke wa Kiislamu na Watoto Wake; Dhati Halisi ya Umma wa Kiislamu!**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi - Halaqa 9**

**SWALI/JAWABU:**
**> Harakati za Urusi na Amerika Nchini Syria**
**> Hariri ni Mfuasi wa Serikali ya Saudi Arabia**




**" WAO NI MAADUI, JIHADHARI NAO. ALLAH AWAANGAMIZILIE MBALI! VIPI WANAPOTOKA NA HAKI? "**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 06/1439 Ijumaa, 27 Rabi' I 1439 H 15/12/2017 M

# "Wao ni maadui, jihadhari nao. Allah awaangamizilie mbali! Vipi wanapotoka na haki?"

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Mnamo Disemba 13/12/2017, viongozi wa nchi hamsini na tano za biladi za Kiislamu walikusanyika jijini Istanbul kujibu uamuzi wa Trump wa kutangaza Al-Quds (Jerusalem) kuwa mji mkuu wa umbile la Kiyahudi, na kama kawaida yao hawaku wavunja moyo Waislamu, wazungumzaji walipitiliza katika kushutumu na kukemea, kwa sababu wao ni vibaraka tu wa wakoloni makafiri wa kimagharibi na vifaa vya vita vyao dhidi ya Uislamu, na juhudi zao za kuwazuia Waislamu kurudi katika maisha kamili ya Kiislamu, na kuhakikisha usalama wa maslahi yao, na kuwaruhusu kufuja rasilimali zetu na kukoloni ardhi yetu.

Na kwa kurudilia taarifa zao, twapata kuwa zote ziliishia tu katika ombi la kutaka kufanywa Jerusalem Mashariki kuwa mji mkuu wa dola "ya kimadai" ya Palestina, kwa mujibu wa maazimio ya ile inayo itwa kanuni ya kimataifa!

Maregeleo yao ni kanuni ya kimataifa, iliyo tungwa na dola za kikoloni za kikafiri, kwa lengo pekee la kuhifadhi maslahi yao ya kikoloni ili kuuangamiza Umma wa Kiislamu baada ya kwisha kuiangamiza Khilafah; wamezigawanya biladi za Waislamu kuwa nchi hamsini na tano zilizo sambaratika zinazo tukuza kanuni ya kikafiri na kupiga vita sheria ya Allah na Mtume wake!

Kwa kitendo hiki, wamedhihirisha utiifu wao kwa mabwana zao, waajiri wao wazuri, nchi za kikoloni. Japo kama ambaye wamejifunga na miito ya shirika lao "Ushirikiano wa Kiislamu" wangetambua kwamba Uislamu unahitaji umoja wa Waislamu chini ya dola moja ikiongozwa na kiongozi mmoja, na sio wengi. Imam Muslim amesimulia hadith kutoka kwa Mtume (saw):

«إِذَا بُويِعَ لِخَلِيفَتَيْنِ، فَاقْتُلُوا الْآخَرَ مِنْهُمَا»

"**Pindi ahadi ya utiifu (Bay'ah) inapopewa makhalifah wawili muuweni huyo wapili miongoni mwao**"

Na hadith yake (saw):

«سَتَكُونُ هَنَاتٌ، وَهَنَاتٌ، فَمَنْ أَرَادَ أَنْ يُفَرِّقَ بَيْنَ أَمْرِ الْمُسْلِمِينَ وَهُم جَمِيعٌ فَاضْرِبُوهُ بِالسَّيْفِ كَائِنًا مَنْ كَانَ»

"**Kutakuweko na mizozo na mivutano, yeyote atakaye taka kuuvunja umoja wa Waislamu; mkateni shingo yake kwa upanga awe atakaye kuwa.**"

Na hadith yake (saw):

«مَنْ أَتَاكُمْ وَأَمْرُكُمْ جَمِيعٌ عَلَى رَجُلٍ وَاحِدٍ يُرِيدُ أَنْ يَشُقَّ عَصَاكُمْ أَوْ يُفَرِّقَ جَمَاعَتَكُمْ فَاقْتُلُوهُ»

"**Yeyote atakaye wajilieni huku mukiwa mumeshikamana pamoja chini ya kiongozi mmoja akataka kuvunja mshikamano wenu au kugawanya umoja wenu, muuweni.**"

Imam Al-Nawawi asema katika "Sharh Muslim": Ni agizo la kumpiga vita yule aliye kwenda kinyume na kiongozi au kutaka kuvunja umoja wa Waislamu na kadhalika, Allah atuepushe mbali, ikiwa hata rudi nyuma anapaswa kupigwa vita, na ikiwa uovu wake hauondoki isipokuwa kwa kifo chake basi anapaswa kuuliwa. Hadith hii ni dalili inayo thibitisha uharamu wa kuwa na zaidi ya Imam mmoja au Makhalifah wawili kwani hili hupelekea mgawanyiko na mfarakano, na kutokea kwa mvutano na kutoweka kwa baraka, hii imepokewa kwa wingi wa upokezi. Asema kuwa wanazuoni wamekubaliana kuwa haijuzu kuteua Makhalifah wawili kwa wakati mmoja."

Sasa twambieni, enyi viongozi na watawala: maregeleo yenu ni kwa sheria ipi, ya Allah au ya maadui wa Allah? Je, inaruhusiwa katika sheria ya Allah "kuweka amani" na Mayahudi kwa kuwapa sehemu kubwa ya ardhi ya Palestina?! Je, sheria ya Allah inaruhusu kuzivunja vunja biladi za Waislamu kuwa vijidola vingi? Au yaagiza kuunganishwa kwao? Munajua fika kuwa pindi Umma utakapo ungana kama dola moja, dola yake itakuwa nambari moja duniani katika nyanja zote, na nchi nyengine zote za kiulimwengu zitatafuta ridhaa yake. Amerika na wengineo hawange subutu kuchukua uamuzi wowote dhidi yake; wala umbile la Kiyahudi lisinge kuwepo.

**Enyi Waislamu:**

Kadhia sio tangazo la Trump kuwa Jerusalem iwe mji mkuu wa dola ya Kiyahudi, huku watawala wa Waislamu wakikusanyika jijini Istanbul, uliokuwa makao makuu ya Khilafah ya Kiuthmani, wito wa kutangazwa Jerusalem Mashariki kuwa mji mkuu wa Gaza na Ukingo wa Magharibi au kile wanacho kiita dola ya Palestina. Wanaitambua Jerusalem Magharibi, bali ardhi yote ya Palestina, kuwa milki ya umbile la Kiyahudi! Lakini kadhia ni kuwa Palestina na Jerusalem yake na miji yake na vijiji vyake vyote ni ardhi ya Kharaji ya Kiislamu milki ya Umma mzima wa Kiislamu mpaka siku ya Qiyama. Ni lazima ikombolewe, na umbile la Kiyahudi kung'olewa,

*Endelea Uk..3*

kwa kupitia majeshi ya Waislamu. Majadiliano ya kisiasa wala mikataba ya muda mrefu au mfupi, wala hata maandamano ya ghasia ya watu wa Palestina, licha ya idadi yao kubwa, sio yatakayo ikomboa Palestina. Bali itakombolewa kupitia jeshi lililojihami kikamilifu lililo shikamana na Uislamu, lenye Iman, mipango, mafunzo, zana nzito, ndege, vifaru, makombora na mitutu.

**Enyi Waislamu**

Watawala hawa wanatekeleza maagizo ya maadui wa Umma huu, kwa kujaribu kuubembeleza kukubali uwepo wa Mayahudi na kuweka amani nao, mkabala wake ni kutambua umbile hili katili kwa dola hafifu ya watu wa Palestina katika Ukingo wa Magharibi na Ukanda wa Gaza na Jerusalem Mashariki. Sio siri kwa yeyote miongoni mwenu, kuwa baadhi yao wanalitambua umbile la Mayahudi, bendera yake inapepea wazi wazi jijini Cairo, Ankara na Amman, na biladi nyenginezo za Waislamu kwa siri.

**Enyi Waislamu**

Watawala hawa wanatekeleza uhalifu dhidi yenu nchini Ash-Sham, Yemen, Libya, Misri, Tunisia, na kwengineko. Wanawatawala kwa mkono wa chuma na silaha, na kuwakataza kujifunga na sheria ya Mola wenu, musiamini urongo wao, wala musiwasaidie katika dhulma zao, musiwasikize wala kuwatii.

**Enyi Waislamu**

Hakuna matarajio kwa watawala hawa. Wale walio onyesha wazi wazi amani kwa umbile hili la Kiyahudi ni wanafiki. Wale wanaodai kutokuwa tayari kuweka uhusiano wao nalo pia ni wanafiki. Wote wamemkhini Allah na Mtume wake na waumini, na kuyageuza majeshi yetu kulinda viti vyao vya utawala na kuhifadhi maslahi ya dola za kikoloni na kuwauweni nyie, badala ya kuyaelekeza kupigana katika njia ya Allah kuzikomboa ardhi za Waislamu zilizo kaliwa, na kueneza Uislamu. Kamwe hakuna matarajio kwao, lakini matarajio baada ya Allah (swt), yako kwenu nyinyi katika kuwang'oa makatili hawa na kuwazuia kutowadhibiti nyinyi, na hamu yenu ya kufikia umoja wenu chini ya kivuli cha Khilafah Rashidah katika njia ya Utume.

Na nyinyi, viongozi wa majeshi ya Waislamu, mushatayarisha jibu la kwenda kumpa Mola wa Mbingu na ardhi atakapo kuulizeni (swt) kuhusu kunyamaza kwenu kimya juu ya khiyana ya watawala hawa wazembe (Ruwaybidha), wakati munaiona khiyana yao wazi wazi, na kushuhudia kasi yao katika kuwatii maadui wa Allah na maadui wenu?
Ama kwa mashekhe na wanazuoni, tunawakumbusha kwamba wao ni warithi wa mitume na kwamba jukumu la kuuongoza Umma huu linaanguka mabegani mwao, kupambana na watawala hawa madhalimu, na kutangaza neno la haki na kulingania utabikishaji kamilifu wa sheria ya Allah. Na kipaumbele ya hili ni kuhuisha ufaradhi wa Jihad, sio tu katika kuzikomboa ardhi zilizo kaliwa, bali pia katika kueneza Uislamu ulimwenguni.

Ewe Allah, tupe ahadi yako ya kusimama kwa Khilafah (Istikhlaf); umakinifu na mamlaka, na ututayarishie watu wanaomiliki nguvu kutupa nusra, na kutuwezesha kuikomboa Bait ul Maqdis na kuitwahirisha kutokana na najisi ya Mayahudi.

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Trump na “Nchi za K**!!!”



Mwehu, Donald Trump alipoulizwa kwanini Marekani haiwapi hifadhi wahamiaji wengi kutoka Haiti na Afrika, alijibu kwa matamshi ya kifedhuli na matusi kwamba hakuwa na haja ya wahamiaji kutoka “**nchi za mashimo ya kinyesi**”. Kisha hakusita kutoa hisia zake kwamba anataka wahamiaji kutoka mahala kama Norway. Akikusudia kuwa angependelea wahamiaji weupe kutoka Ulaya badala ya wahamiaji wa kiafrika.

Marekani na Ulaya zimetengeneza utajiri mkubwa kwa kuwatawala kwa ukoloni na kuwafanya watumwa watu wa Afrika na Haiti. Kutoka mwaka 1824 mpaka 1947, Ufarasa iliitenza nguvu nchi ya Haiti kulipa karibu mara kumi ya kipato cha nchi ya Haiti cha mwaka kwa ajili ya kuulipia kinachodaiwa ‘uhuru’ wake. Deni hilo la kujiua la miaka 125 kulipia kinachoitwa uhuru limekiacha kijinchi hiki cha Carribean katika mangamizi makubwa ya kiuchumi. Makampuni ya kimarekani kama Disney yamekuwa yakiinyonya nchi ya Haiti kupitia kuwalipa wafanyakazi wa nchi hiyo kipato kidogo mno ili kuzalishia bidhaa nyingi kwa ajili ya Marekani. Haiti ni mfano hai wa nchi nyingi ulimwenguni zinavyoendelea kuangamia kwa unyonyaji wa ubepari.

Hali ya kuzingatia rangi ya ngozi, utaifa nk. wa wahamiaji ni kielelezo cha kuonesha wazi uovu uliokubuhu wa Ubepari na namna unavyowazingatia wanadamu.

Wahamiaji waliokwenda Madina walikuwa wamo waarabu, waafrika, maskini na matajiri. Kitu pekee kilichowaunganisha na kuwafunga pamoja ni kushikamana kwao na mfumo mmoja wa Uislamu ambao haukuwagawa wala kuwatofautisha kwa msingi wa rangi za ngozi wala msingi wa kipato cha kiuchumi.

Hali ya ubepari ya kumzingatia mtu kwa mujibu wa rangi ya ngozi yake na hali yake ya kiuchumi inadhihirisha wazi kwamba fikra za ubepari si za kila mtu, bali ni za watu maalumu wa tabaka la ‘walio bahatika’.

Uislamu ndio mfumo mbadala wa ubepari, ambao unawazingatia wanadamu wote kuwa sawa, awe mtu rangi yoyote atakayokuwa, na kamwe hauwakadirii wengine kuwa “nusu watu” wasiostahiki haki ya kuhifadhiwa na maendeleo.

يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِنْ ذَكَرٍ وَأُنْثَى وَجَعَلْنَاكُمْ شُعُوبًا وَقَبَائِلَ لِتَعَارَفُوا إِنَّ
أَكْرَمَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ أَتْقَاكُمْ إِنَّ اللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ

**“Enyi watu! Hakika Sisi Tumekuumbeni kutokana na mwanamume na mwanamke. Na tumekujaalieni kuwa mapote na makabila ili mpate kujuana. Kwa hakika aliye mtukufu zaidi kati yenu kwa Mwenyezi Mungu ni aliye mchaMungu zaidi miongoni mwenu. Kwa hakika Allah ni Mjuzi na Mwenye khabari”** [Al-Hujaraat: 13]

**Imefasiriwa kutoka Ukurasa wa Facebook wa Hizb ut Tahrir Amerika**
**https://www.facebook.com/HTAmerica/**

# Nidhamu ya Kijambazi Inayo Wapora Raia Wake

**Habari:**

Watumizi wa umeme wanakabiliwa na deni la bili za nyuma la shilingi 8.1 bilioni huku kampuni ya Kenya Power ikichukua hatua za kumudu gharama za matumizi ya mafuta ya dizeli katika mitambo ya uzalishaji umeme za mwaka jana na ambazo haziku jumuishwa katika malipo ya kila mwezi huku serikali ikigharamia mahitaji ya umma katika mwaka wa uchaguzi. Kenya Power ilidhihirisha kuwepo na mzigo mkubwa wa gharama zake katika taarifa yake ya fedha ya kila mwaka, ikieleza kuwa hii ilitokamana na ukame mkali mwaka jana, iliyopelekea udharura wa ongezeko la uzalishaji ghali wa umeme kwa njia ya dizeli uliofidia upungufu mkubwa wa uzalishaji umeme kwa njia ya maji. Gharama hii ni sehemu ya shilingi 10.1 bilioni zilizo tambuliwa kama gharama za mafuta katika uzalishaji umeme ambazo bado kampuni ya serikali ya Kenya Power haijazirudisha katika taarifa yake ya fedha ya kila mwaka ya mwezi Juni 2017. Takriban shilingi 2 bilioni zimerudishwa kufikia sasa, huku shilingi 8.1 bilioni zikisukumiwa wateja katika bili zao za kila mwezi.

**Maoni:**

Punde tu baada ya tangazo la Kenya Power kuhusu mipango ya kurudisha kiasi hicho cha gharama, takriban jumla ya Wakenya walijibu kwa njia ya kutoridhika katika mitandao ya kijamii kupitia anwani **#switchoffKPLC** dhidi ya mipango hiyo na kila mmoja wao alikashifu wazo kuhusu jinsi gharama hiyo kubwa ilivyo patikana! Serikali ya Kenya kupitia Waziri wa Kawi Charles Keter baada ya kutambua kuwa ripoti iliyotolewa na Kenya Power; haikupokewa vyema na umma ilijiingiza kwa upole kuokoa sura ya serikali ambayo huenda ikakabiliwa na mashtaka mahakamani juu ya hilo. Bwana Keter alisema kwamba kubadilika badilika kwa malipo katika gharama za umeme kuliko hisiwa na wateja hivi majuzi **kulitokana na kuwepo kwa mfumo wa utoaji bili usiokuwa madhubuti unaofanya usomaji wa mitambo ya mita kwa njia ya ukisiaji tu badala ya kuchukua vipimo halisi!**

Kutia msumari kidonda, serikali ilifichua kwamba bili za umeme kwa wananchi wenye pato la chini huenda zikaongezeka kuanzia Aprili 2018 huku malipo kwa wenye mapato wastani yakitarajiwa kushuka kwa kutarajiwa kumalizika kwa ruzuku kwa wateja wadogo! Kwa sasa serikali imewagawanya raia katika vigawanyo vifuatavyo:

1. Watumizi wa chini hutumia nyuzi 50 kwenda chini kwa mwezi na wanalipishwa shilingi 2.50 kwa nyuzi (kWh) moja kwa saa.

*Endelea Uk..6*

2. Watumizi wastani hutumia baina ya nyuzi 51 – 1,500 kwa mwezi na wanalipishwa shilingi 12.75 kwa nyuzi

3. Watumizi wa juu hutumia 1,500 na kwenda juu kwa mwezi na wanalipishwa shilingi 20.57 kwa nyuzi

Taarifa hizo za juu zinathibitisha kuwa katika nchi yoyote ya kirasilimali utoaji huduma ni njia ya biashara na wala sio jukumu jumla kwa serikali yoyote juu ya raia wake. Iweje kampuni ya serikali mithili ya Kenya Power itangaze **faida ya shilingi 7.27 bilioni** huku raia ambao walitakiwa wawe wamiliki wa kampuni hii wanateseka juu ya malipo makubwa kwa msingi wa vigawanyo hivi ambavyo hakukuwa na usemi wao katika kuundwa kwake? Jibu ni makampuni katika serikali za kirasilimali yanajulikana kumilikiwa na serikali katika waraka pekee lakini kiuhalisia, yanasimamiwa na kuendeshwa na warasilimali walafi kwa jina la **wawekezaji**. Wanaoitwa wawekezaji ndio wanao dhibiti taasisi za kiserikali na kutekeleza sera zinazo kusudia kuwapendelea wao na kuhakikisha kuwa wanapata migao ya juu ya faida kutokana na hisa wanazomiliki. Hii imepelekea raia kuteseka katika sekta zote mfano ikiwemo ya afya ambapo raia wasiokuwa na bima kama ile ya afya ya kitaifa almaarufu NHIF hawakubaliwi au kutibiwa katika mahospitali, sera za elimu huundwa kuwapendelea wawekezaji katika sekta hiyo kiasi ya kuwa elimu bora kamwe sio kigezo kinachotumiwa katika upimaji sera!

Suluhisho la kipekee ni kubadilisha nidhamu hii ya kijambazi ya kidemokrasia na mfumo wake batili wa kirasilimali inayotokamana kwayo. Nidhamu inayo nawiri kupitia kuwafanyia unyama raia wake na kutazama utoaji huduma kama chimbuko la pato na miradi kuundwa ili kufuja mali ya umma kwa ajili ya maslahi ya kibinafsi. Kulingania kubadilishwa kwa nidhamu aina hiyo sio tu ni kadhia ya dharura bali ni hitajio litakalo leta amani, utulivu na ufanisi kwa raia wote ambao kamwe hawata gawanywa kwa msingi wa mapato yao. Hilo laweza pekee kupatikana chini ya nidhamu adilifu ya utawala iliyojengwa kutokana na mfumo safi wa Kiislamu kwa Njia ya Mtume (saw). Khilafah (nidhamu ya utawala ya Kiislamu) daima itakuwa inajitahidi kumridhisha Allah (swt) na kuwa na hamu ya baraka zake na rehma zake ili kuingizwa katika pepo yake ya juu. Kwa kuzingatia hilo, watawala ndani ya Khilafah watashajiishwa kwa utoaji hudumu halisi na kilicho cha Umma kitatambuliwa kwa uhalisia kuwa cha Umma na kutumiwa na kupewa kipaumbele kukidhi mahitaji ya raia kwa msingi wa maoni yao.

**Enyi Wakenya**, mpaka lini mutateseka kutokana na usaliti huu wa kiuchumi kutoka kwa serikali yenu wenyewe? Huu ni unyama kuona kuwa maisha yenu daima yamejaa mateso; licha ya mishahara duni ambayo wachache wenu walio bahatika kuajiriwa wanapokea; bado wanapanga njama ya hata kukichukia hicho kidogo munacho kihifadhi kupitia ushuru wa kila aina ambao mumeangaziwa kwao? Tunawalingania kutafakari kwa makini juu ya hali muliyoko nayo kwa sasa na mustakbali wa watoto wenu na wajukuu zenu na kisha mujiulize nafsi zenu; je, hakuna suluhisho msingi la kudumu? Kwa moyo mkunjufu tunazielekeza nyoyo zenu na akili zenu zilizo na ikhlasi kuupa Uislamu fursa na kuusoma kama mfumo ulio teremshwa kwa Mtume Muhammad (saw) ili kuendesha mambo yote ya maisha ya wanadamu kwa mfumo huo.

**Enyi Waislamu,** mpaka lini mutashabikia nidhamu iliyo kinyume na yale yaliyo teremshiwa kipenzi chenu Rasulullah (saw)? Je mumetosheka pekee na vibahashishi ambavyo mfumo huu muovu na batili wa kirasilimali unawarushia mikononi mwenu na kutupilia mbali furaha ya milele katika mabustani ya Jannatul Firdaus? Sisi ndugu zenu tumefungua mikono yetu na kuwalingania katika kazi iliyo bora zaidi iliyo tawazwa kwa Mitume ya kuongoza Umma kutoka katika giza kwenda katika nuru. Giza la utawala wa kirasilimali na itikadi yake ya kiilamaniy iliyo sababisha leo majanga ya kila siku duniani. Ili kwa pamoja tulinganie badali ya giza hili kuwa nuru ya Uislamu kama mfumo utokao kwa Muumba wa mwanadamu. Nuru itakayo angaza majumba yote yakiwemo majumba ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu kutokana na rehma za Muumba kwa viumbe vyake.

**Ali Nassoro**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

http://www.nation.co.ke/news/Why-Sh8-1bn-has-been-slapped-on-power-bills-/1056-4251366-6xw93hz/index.html

http://www.nation.co.ke/news/Electricity-bills-will-not-be-backdated-Energy-CS-Charles-Keter/1056-4255806-yok4mdz/index.html

http://www.nation.co.ke/news/Poor-homes-to-pay-more-for-electricity/1056-4256474-oos5asz/index.html

# Siku Aliyo Lia Mtume (Rehema na Amani Zimshukie)

Kutoka kwa Ibn Masoud (ra) amesema: Mtume Rehema na Amani za Mwenyezi Mungu zimshukie aliniambia: “Hebu nisomee Quran”. Nikamwambia: ‘Ewe Mtume wa MwenyeziMungu nikusomee na kwako ndio imeteremshwa? Akasema Mtume (saw): “Hakika mimi napenda niisikie kwa mtu mwengine”. Ibn Masoud Akasema; Nikamsomea surat Nisai hadi kufikia aya hii:

فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِن كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيداً

**Basi itakuwaje tutakapoleta shahidi katika kila umma na tutakuleta wewe (Nabii Muhammad) uwe shahidi juu ya huu umma wako.** [An-Nisaa: 41]

Hapa Mtume (saw) akamwambia Ibn Masoud: “Tosha” Mara nikimgeukia nikaona akitiririkwa na machozi usoni mwake.

Kikawaida kwa mwenye kuisoma Quran na kuzingatia maana yake basi moyo wake hulainika kwa kujawa na Khofu ya Mola wake. Kitendo cha Mtume (saw) kumtaka swahaba wake Ibn Masoud (ra) amsomee Quran, kinaelezewa na wanavyuoni kwamba wakati mwengine Quran humuathiri mtu zaidi pale anapo isikiliza kwa mwenzake. Twaona jinsi gani Mtume (saw) alivyo shindwa kuhimili kilio alipo isikiza aya hii ishara ya kuwa Quran sio kitabu tu cha kusomwa tu bali inatakikana kuwe na athari na mazingatio makubwa kila tunapo isoma. Katika fitina kubwa wamagharibi waliofaulu kufitini Waislamu ni kuondosha ndani ya mabongo yao ufahamu halisi wa Quran. Huyu hapa waziri wa zamani wa Uingereza Disrael akisema kwamba; ‘**Njia pekee ya kuwamaliza Waislamu ni kutoa ufahamu wa Kitabu hiki (Quran) ndani ya mabongo yao**’. Kwa kifupi akiashiria kuwa mafunzo yaliyomo ndani ya Quran yachukuliwe kama nadharia na falsafa tu zisizowezekana katika maisha ya kila siku. Na naam hapa ndio tumefikia, misikiti imejaa tele misahafu huku watu wakiweka halaka za tafsiri ambazo huishia kuambizana tu pasina kufanyia kazi.

Ni muhimu kuzingatia kilio cha bwana Mtume (saw) hasa kwenye maana ya aya hiyo ya Surat An-Nisai. Bila shaka aya inataja siku nzito ya Qiyama ambayo miongoni mwa hali zake ngumu ni kama ilivyo tajwa kwenye aya iliofuata baadaa ya hiyo iliomliza bwana Mtume (saw) yaani ya nambari 42 Mola akisema:

يَوْمَئِذٍ يَوَدُّ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَعَصَوُاْ ٱلرَّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ بِهِمُ ٱلأَرْضُ وَلاَ يَكْتُمُونَ ٱللَّهَ حَدِيثاً

**Siku hiyo walio kufuru na wakamuasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao. Wala hawataweza kumficha Mwenyezi Mungu neno lolote.** [An-Nisaa: 42]

Tukiachilia mbali huruma ya Mtume (saw) kwa umma wake twaweza tukasema kilichompelekea kuangua kilio ni ushuhuda wake mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa Umma wake na uliotangulia. Na hii ni kama ilivyo pokewa kuwa siku ya Qiyama Kila nabii atakuja akiwa na mtu mmoja na nabii mwengine awe na watu wawili bali na zaidi ya hao. Watu wake waitwe mbele yake waulizwe: ‘Je, huyu nabii wenu aliwafikishia ujumbe?’ Watu waseme, ‘La’. Kisha yule nabii aulizwe: ‘Je, uliwafikishia ujumbe hawa watu?’ Nabii aseme; ‘Ndio’. Kisha aambiwe, ‘ni nani shahidi wako?’ aseme, ‘Muhammad na Umma wake’. Mtume (saw) na Umma wake waulizwe: ‘Je, aliwafikishia nabii huyu watu wake ujumbe?’ Waseme: ‘Ndio’. Kisha uulizwe, ‘nyinyi mlijuaje?’ Waseme: ‘Alitujiliia Mtume (saw) akatueleza kwamba mitume iliwafikishia watu wao ujumbe’.

Tukitaamali zaidi tutakuta maswali msingi hapa: -

Je, kweli Mtume (saw) alifikisha Uislamu kama mfumo kamili kwa umma wake? Jawabu ya haraka na iso na shaka ni; ndiyo, Sasa swali ni Je, sisi Waislamu kweli tumeuchukua Uislamu kimfumo kamili na kama nuru aliyo kuja nayo (saw) ama tumetabani mfumo mwengine uso na mashiko na wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt). Jawabu ni kuwa Waislamu leo hatuko chini ya Nuru aliyo kuja nayo Mtume wetu (saw). Siasa zetu, uchumi na nidhamu ya kijamii zote hizo tunazipeleka kwa mujibu wa ukafiri wa Kirasilimali. Wengi wetu tumeingizwa khofu tukiogopa lawama ya wasemao kuwa Uislamu ni mfumo muovu bali usojimudu karne hii! Bali la kutia uchungu zaidi ni kuwakatisha tamaa wachache miongoni mwetu na kuwakejeli kila wanao kumbwa na vitimbi vya madhalimu kwenye kazi tukufu ya kuukomboa ulimwengu upya kupitia kusimamisha Uislamu ndani ya serikali yake ya Khilafah. Je, hali itakuwaje siku hiyo ikiwa hivi sasa Uislamu tumeugeuza juu chini?

Na hapa ni tujitambue sisi kama Waislamu kuwa mbele yetu ipo kazi ya kushikamana na Uislamu kama alivyo tuachia Mtume wetu (saw). Tuzingatie kuwa kama atakavyo kuwa shahidi Mtume wetu (saw) pia nasi ni mashahidi kwa watu wengine. Na hii ni kama Mwenyezi Mungu (swt) alivyosema:

وَكَذَٰلِكَ جَعَلْنَاكُمْ أُمَّةً وَسَطاً لِّتَكُونُواْ شُهَدَآءَ عَلَى ٱلنَّاسِ وَيَكُونَ ٱلرَّسُولُ عَلَيْكُمْ شَهِيداً

**Na vivyo hivyo tumekufanyeni muwe Umma wa wasitani (adilifu), ili muwe mashahidi juu ya watu, na Mtume awe ni shahidi juu yenu.** [Al-Baqarah: 143]

Kwenye ayah ni kwamba sisi ndio Umma bora kwani tupo kwenye mfumo wa kweli na wenye uadilifu na ndio maana sisi ni mashahidi kwa Umma nyengine kwa sababu tuko kwenye uadilifu. Na kama inavyo julikana katika sharuti za ushuhuda huwa ni uadilifu. Kwa namna hii basi bila shaka tumekalifishwa na MwenyeziMungu (swt) kuwafikishia

Endelea Uk..8

watu suluhisho ya matatizo yao yote yakiwemo ya kisiasa, uchumi na kijamii. Tusipo fanya hivyo tutakuwa tumehatarisha maisha yetu hapa duniani na kesho Mtume (saw) ataeleza bayana kuwa sisi tulikengeuka ujumbe wake tukaishi kinyume na Uislamu aliokuja nao yeye (saw).

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**



# Mwanamke wa Kiislamu na Watoto Wake; Dhati Halisi ya Umma wa Kiislamu!

Bila shaka yoyote watoto ni chimbuko la furaha na ridhaa kuu; huyafanya maisha kuwa matamu, na huleta matumaini. Baba huwaona watoto wake kuwa chimbuko la usaidizi wa siku za usoni, pamoja na kuwakilisha ongezeko la idadi na kudumu kuendelea kwa familia. Mama huwaona watoto kuwa chimbuko la matumaini, maliwazo na furaha maishani, na kama matarajio siku za usoni. Matarajio yote haya yanategemea malezi mazuri ya watoto hawa na kuwapa matayarisho muwafaka kwa maisha, ili wawe watu wakakamavu na wenye kuleta faida ndani ya mujtamaa, chimbuko la kheri kwa wazazi wao, jamii na mujtamaa kwa jumla. Ndipo watakapo kuwa kama vile Allah (swt) alivyo wafafanua:

**((...الْمَالُ وَالْبَنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا))**

**(Mali na watoto ni mapambo ya maisha ya dunia . . .)** (Al-Kahf:46)

Ikiwa elimu na malezi yao yatapuuzwa, watakuwa na utambulisho ‘shakhsiyya’ mbaya, mzigo kwa familia yao, jamii na mujtamaa kwa jumla. Hivyo basi mama ni sharti aelewe jukumu kubwa alilo nalo juu ya watoto wake.

Mwanamke wa Kiislamu kamwe hasahau kuwa jukumu la mama katika malezi ya watoto na kuunda utambulisho ‘shakhsiyya’ wao ni kubwa zaidi kuliko jukumu hilo kwa baba, hii ni kwa sababu kimaumbile watoto huwa karibu sana na mama yao na hutumia muda mwingi wakiwa pamoja naye; hivyo basi anajua yote kuhusu tabia zao, hisia zao ukuaji wa kifikra utotoni mwao na katika kipindi kigumu cha kubaleghe kwao.

Hivyo basi, mwanamke anayefahamu mafundisho ya Uislamu na jukumu lake binafsi la kuwa mwalimu maishani, hujua jukumu lake kamili la malezi ya watoto wake, kama lilivyo elezwa ndani ya Qur’an:

**يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنْفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا))**
**((...وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ**

(Enyi mulio amini! Ziokoeni nafsi zenu na za jamaa zenu na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe . . .) (At-Tahreem:6)

Imepokewa na Abdullah ibn ‘Umar (ra) Mtume (saw) pia amelieleza jukumu hili katika hadith hii:

**عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ عُمَرَ يَقُولُ: سَمِعْتُ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّه عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَقُولُ: ((كُلُّكُمْ رَاعٍ وَكُلُّكُمْ مَسْؤول عَنْ رَعِيَّتِهِ، الإِمَامُ رَاعٍ وَمَسْؤولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ، وَالرَّجُلُ رَاعٍ فِي أَهْلِهِ وَهُوَ مَسْؤولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ، وَالْمَرْأَةُ رَاعِيَةٌ فِي بَيْتِ زَوْجِهَا وَمَسْؤولَةٌ عَنْ رَعِيَّتِهَا، وَالْخَادِمُ رَاعٍ فِي مَالِ سَيِّدِهِ ومَسْؤولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ...))**

**“Nyote ni wachungaji na nyote mutaulizwa juu ya mulivyo vichunga, kiongozi ni mchungaji na ataulizwa kuhusu raia wake, na mume ni mchungaji wa familia yake na ataulizwa kuwahusu, na mke ni mchungaji wa nyumba ya mumewe na ataulizwa kuihusu, na mtumishi ni mchungaji wa mali ya bwana wake na ataulizwa kuihusu...”**

Uislamu umeweka jukumu juu ya mabega ya kila mtu; hakuna yeyote aliye achwa pasi na majukumu. Wazazi – hususan mama – wamefanywa kuwa wasimamizi katika kuwapa watoto wao malezi imara na elimu sahihi ya Kiislamu, kwa msingi wa sifa alizotangaza Mtume (saw) kuwa ametumilizwa kwa ajili ya kuzikamilisha na kuzieneza miongoni mwa watu:

**(( إنما بعثت لأتمم مكارم الأخلاق ))**

“**Hakika nimetumilizwa ili nikamilishe tabia njema.**”

Hakuna kinacho ashiria zaidi ukubwa wa jukumu la wazazi kwa watoto wao na wajibu wao wa kuwapa malezi sahihi kuliko hukmu ya maulama kuwa kila familia itilie maanani maneno ya Mtume (saw):

**مُرُوا أَوْلادَكُمْ بِالصَّلاةِ وَهُمْ أَبْنَاءُ سَبْعِ سِنِينَ ،))**
**((وَاضْرِبُوهُمْ عَلَيْهَا وَهُمْ أَبْنَاءُ عَشْرٍ**

*Endelea Uk..9*



Email: info@uqab.or.ke

“**Waamrisheni watoto wenu kuswali wanafika umri wa miaka saba, na wapigeni juu ya hilo wanapofika umri wa miaka kumi.**”

Wazazi wowote wanao fahamu hadith hii lakini wakawa hawawafundishi watoto wao kuswali wanapofikia umri wa miaka saba au kuwapiga ikiwa hawataswali wanapofikia umri wa miaka kumi, ni wazazi waliomo kwenye madhambi na waliofeli katika jukumu lao; wataulizwa mbele ya Allah (swt) kwa kufeli kwao huku.

Nyumba ya familia ni taswira ndogo ya mujtamaa ambamo akili za watoto, fikra zao, hisia zao na matamanio yao huundwa wakati ambapo wangali wachanga na wako tayari kupokea maneno sahihi ya uongofu. Hivyo basi dori muhimu ya wazazi katika kuunda akili za watoto wao wa kiume na wa kike na kuwaongoza katika haki na amali njema iko wazi.

Wanawake wa Kiislamu daima wamekuwa wakifahamu jukumu lao katika malezi ya watoto wao, wanarekodi nzuri sana katika upande wa kuzalisha na kuathiri wanaume watukufu, na kutia ndani ya nyoyo zao maadili mema. Hakuna ushahidi mkubwa wa hili kuliko ukweli kuwa wanawake werevu na mahiri wameweza kuzalisha watoto waheshimika zaidi kuliko wanaume werevu na mahiri, kiasi ya kuwa huwezi kupata yeyote miongoni mwa wanaume watukufu wa Umma wetu walioweza kutawala matukio ya kihistoria ambaye hakuupata utukufu wake kupitia mamake.

Al-Zubayr ibn al-’Awwam (ra) anarudisha shukrani zake kwa mamake Safiyyah bint ‘Abd al-Muttalib (ra) kwa utukufu wake, ambaye alikuuza ndani yake sifa nzuri na maumbile ya kipekee.

‘Abdullah, al-Mundhir na ‘Urwah, watoto wa al-Zubayr (ra) ni matunda ya maadili yaliyo kuzwa ndani yao na mama yao, Asma’ bint Abi Bakr (ra), na kila mmoja wao aliweka alama katika historia na kupata daraja ya juu.

‘Ali ibn Abi Talib (ra) alipata hekima yake, tabia njema na shakhsiyya njema kutoka kwa mamake maarufu, Fatimah bint Asad.

‘Abdullah ibn Ja’far (ra), bwana wa ukarimu wa Waarabu na kiongozi wao muheshimiwa zaidi, alimpoteza babake akiwa na umri mdogo, lakini mamake Asma’ bint ‘Umays (ra) alimlea kwa uangalifu na kumpa maadili na utambulisho ‘shakhsiyya’ mwema iliyopelekea mpaka yeye mama kuwa miongoni mwa wanawake watukufu katika Uislamu.

Pia, historia imenakili majina ya wanaume wawili watukufu kutoka kabila la Banu Umayyah, wa kwanza alijulikana kwa shakhsiyya yake imara, uwezo, werevu, hekima na azma, na wa pili alichukua njia ya uadilifu, kheri, ucha Mungu na wema.

Wa kwanza ni ‘Abd al-Malik ibn Marwan (ra), ambaye mamake alikuwa ni ‘A’ishah bint al-Mughirah ibn Abi’l-’As ibn Umayyah, ambaye alikuwa maarufu kwa shakhsiyya yake imara, azma na werevu wake. Wa pili ni ‘Umar ibn ‘Abd al-’Aziz (ra), wa tano miongoni mwa Makhalifah waongofu, ambaye mamake alikuwa Umm ‘Asim bint ‘Asim ibn ‘Umar ibn al-Khattab (ra), aliyekuwa na shakhsiyya tukufu zaidi miongoni mwa wanawake wa zama zake. Mamake alikuwa mja mwema aliye muabudu Allah (swt) ambaye ‘Asim aliona ndani yake uaminifu na ukweli, na kufuata kwake njia ya sawa wazi wazi, pindi alipokataa kuongeza maji kwenye maziwa kama alivyo agizwa na mamake, kwa sababu alijua kuwa Allah (swt) anamuona.

Tunapogeukia Andalusia (Spain), tunamkuta kiongozi mahiri, mwenye maono ‘Abd al-Rahman al-Nasir ambaye, licha ya kuanza maisha akiwa yatima, aliweza kupanua mipaka ya dola ya Khilafah na kufika mpaka Magharibi, ambapo iliwafanya viongozi na wafalme wa bara Ulaya kujisalimisha kwa dola hiyo na dola ambayo taasisi zake za kielimu ziliweza kuzalisha wasomi na wanafalsafa kutoka katika mataifa yote yaliyokuja kutafuta elimu. Dola hii ilitoa mchango mkubwa kwa hadhara ya Kiislamu ulimwenguni. Ikiwa tutafanya utafiti juu ya siri ya utukufu wa mwanamume huyu, tutakuta kuwa unatokana na utukufu wa mamake aliye fahamu jinsi ya kukuza maadili makuu ya kuwa mtu mwenye maono.

Katika zama ya utawala wa ‘Abasiyya walikuweko wanawake wawili watukufu waliopanda mbegu za maono, utukufu na nguvu kwa watoto wao. Wa kwanza alikuwa mamake Ja’far ibn Yahya (ra), aliyekuwa Waziri wa Khalifah Harun al-Rashid. Wa pili alikuwa mamake Imam Shafi’: ambaye hakuwahi kumuona babake aliyefariki akiwa mchanga; mamake ndiye aliyemlea kwa uangalifu na kumsomesha.

Kuna mifano mingi ya aina hii ya wanawake katika historia yetu, wanawake walioweza kukuza katika watoto wao, shakhsiyya heshimika na mbegu za utukufu, na ambao walisimama kidete nyuma yao kwa kila walichopata katika utawala na cheo.

Vile vile hili liwe kwa wanawake na mama wa Kiislamu leo, hawana budi kusimama kidete kutekeleza majukumu yao na kuchukuwa mfano kutoka kwa watangulizi wao katika kuunda Umma wa Kiislamu ulio imara kwa kupitia kuwalea watoto wao wa kiume na wa kike kwa thaqafa imara ya Kiislamu. Hawana budi kutia motisha ndani ya nyoyo za watoto wao wa kushikamana imara na dini yao na da’wah ya Kiislamu hususan da’wah ya kurudisha Uislamu kama mfumo kamili wa maisha kupitia kusimamisha dola ya Kiislamu ya Khilafah, dola ambayo ndiyo iliyo zalisha mama na watoto waliotangulia kutajwa juu kama watu waliokuwa na shakhsiya heshimika za kipekee katika historia yote ya Uislamu.

**Masoud Salim Mazrui**
**Mwanachama wa Hizb ut Tahrir Kenya**

# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 9: Kuvumilia Shida na Maudhi kwa Abdullahi Ibnu Masoud na Mus'ab Ibnu Umair Katika Da'wah



Katika halaqa hii tutamalizia mbinu ya nne na ya mwisho ambayo wameitumia Maquresh dhidi ya da'wah ya Mtume (saw). Na leo tutazungumzia maudhi na adhabu ambazo wamezipata baadhi ya Maswahaba Radhi za Allah ziwaendee.

**Wa kwanza aliye dhihirisha Uislamu**

Ameelezea Zubeyr ibnul Awwam (ra) asema: Wa kwanza aliye dhihirisha Uislamu baada ya Mtume (saw) katika mji wa Makkah ni Abdullah Ibnu Masoud (ra) walipo kusanyika maswahaba wa mtume (saw) wakasema: Maquresh hawajaisikia Qur'an ikisomwa wazi kabisa. Je Nani atawasikilizisha? Akasema Abdullah Ibnu Masoud: Mimi
Wakasema: Sisi tunakuogopea, sisi tunataka mtu ambaye ana jamaa watakao mhami kutokana na hawa watu wakitaka kumfanyia ubaya.... Akasema: Niacheni Allah Atanihami...! Kesho yake Ibnu Masoud alipo pambaukiwa Alikuja katika Maqam wakati wa dhuha/ asubuhi na Maqureysh wako katika shughuli zao. Akasimama katika Maqam kisha akasoma kwa sauti juu aya hii:

الرحمن علم القرآن

**Mwingi wa Rehma, Amefundisha Qur'an.** [Ar-Rahmaan: 2]

Kisha akawaelekea huku anasoma wakasikiza kwa makini huku wanasema: Anasema nini mtoto wa mama mtumwa…? Hakika anasoma baadhi ya aliyo kuja nayo Muhammad... wakamwenukia wakawa wanampiga usoni mwake, na yeye anaendelea na kisomo chake mpaka akafika katika kisomo kiasi Allah anachotaka afike...

Kisha akarudi kwa maswahaba (ra) wenzake ilhali amepigwa usoni mwake na katika mwili wake, wakamwambia: haya ndio tuliyo kuwa tunayaogopea kwako...! Akasema: Maadui wa Allah hawaja wahipo kuwa madhalili kwangu kuliko sasa, na mkitaka kesho pia nitawaendea...! Wakasema: hapana tosha hiyo kwani umewasikilizisha wanachokichukia...!

**Balozi wa kwanza wa Uislamu**

Mus'ab Ibnu Umair, ni mmoja wapo miongoni mwa wale waliofundishwa adabu na Uislamu, na akalelewa na Muhammad (saw). Hakika kisa cha maisha yake yana Sharaf kubwa kwa wanadamu...!

Alisikia kuwa Rasul (saw) na walio pamoja naye wanajumuika katika nyumba ya Arqam Ibnu Abiy Al-

*Endelea Uk..11*

Arqam, Akaenda huku ana mahaba, na kwa upepesi wa jicho akasilimu na akamficha mamake Uislamu wake...!

Alionekana na Uthman Ibnu Twalha akiingia katika nyumba ya Arqam kwa kujificha kisha akaonekana tena mara ya pili akiswali kama swala ya Muhammad (saw) huyu bwana akaenda upesi kumpa habari mamake. Kwa haraka mama akatangaza kukasirishwa kwake na Mus'ab kwa sababu Ameigura miungu.

Alisimama Mus'ab mbele ya mamake na jamaa zake na mbele ya mabwenyenye wa kiquraysh walio kusanyika mbele yake akawasomea Qur'an kwa yakini na thabat ambayo Muhammad (saw) huosha mioyo yao nayo na kujaza kwayo hikma na nguvu, sharaf na uadilifu na uchamungu...!

Alikuwa Mus'ab kabla ya kusilimu kwake ni kijana anaye julikana mwenye neema aliye zaliwa katika neema na akakulia katika neema, na akawa barobaro katika hali hii. Mamake alipokata tamaa ya kuritadi kwake alimnyima kila kitu alichokuwa akimpa, akakataa asile chakula chake mtu aliye igura miungu, akamlaani, hata kama huyu mtu ni mtoto wake...!

Si haya tu, bali aliendelea mamake na vikwazo akamfungia katika chumba akawa humo mahabusu, mpaka walipotoka baadhi ya Waumini wakigura kwenda Habasha naye akajitolea na kuwahepa walinzi na mamake, akaenda Habasha...!

Mus'ab aliiandaa nafsi yake abadili maisha yake kwa maisha mapya ambayo muongozo wake amepewa na Muhammad (saw). Alitoka siku moja na baadhi ya Waislamu wakiwa wamekaa kando ya Mtume (saw) walipo muona wakainamisha vichwa vyao na kufumba macho yao wengine wakatokwa na machozi mengi sana hilo ni kwa kumuona Mus'ab amevaa joho lenye viraka wakakumbuka hali aliyokuwa nayo mwanzo kabla ya kusilimu, alipokuwa na nguo kama maua na bustani inayopendeza na mafuta mazuri yanayonukia…!

Alipo muona (saw) alisema: "**Nilimuona Mus'ab huyu, na Makkah hakukuwa na kijana aliye pata neema/ mazuri kwa wazazi wake kama yeye, na amewacha yote hayo kwa mapenzi ya Allah na Mtume wake...!**"

Kisha Mtume (saw) akamchagua kwa jukumu muhimu...! Alimchagua awe balozi kwa mji wa Madina, anawafundisha Maanswar ambao walimpa bay'ah katika Aqabah na kuwaingiza wengine katika dini, na kuiandaa Madina kwa siku ya Hijra kubwa.

Alifaulu Mus'ab Ibnu Umair kufaulu kuso na mfano! Alienda Madina siku aliyotumwa na Rasul (saw) na Madina hamna Waislamu isipokuwa 12 tu lakini yeye alikaa nao miezi ya kuhesabika mpaka wakakubali watu wa Madina mwito wa Allah na Mtume wake (saw), hakukubakia nyumba katika mji wa Madina ila kunatajwa Uislamu ndani yake...!

Na katika msimu wa Hijjah uliofuatia bay'ah ya Aqabah Waislamu wa Madina walikuwa wakituma wajumbe wanao wawakilisha... Na ikawa idadi ya Wanachama ni kundi la Waumini sabiini na mwanamke mmoja (71) walihudhuria kutekeleza amali za Hijjah, waliulizana wao kwa wao: "mpaka lini tutamuacha Mtume (saw) anafukuzwa kwenda katika majabali ya Makkah na akiogopa...?

Walipofika Makkah kukapita kati yao na Mtume (saw) mawasiliano ya kisiri yaliyo pelekea baya'h ya Aqabah ya Pili ambayo ilijulikanwa baada ya hapo kuwa ni **Bay'atul Harb**.Hii ilikuwa kabla ya kusimama serikali ya Kiislamu.

Baada ya kusimama serikali ya Kiislamu chini ya Uongozi wa Mtume (saw), Mus'ab (ra) alibeba bendera siku ya Uhud, Waislamu walipolemewa yeye alibaki uwanjani, Ibnu Qumaiah alimfuata akampiga Mus'ab mkono wa kulia na kuukata, Akashika bendera kwa mkono wa kushoto nao pia ukakatwa, Akashika bendera kwa vigutu na akaibana kwa kifua chake...! Mara ya tatu akampiga kwa mkuki bendera ikaanguka ikapaa roho ya Mus'ab kwenda katika Jannah ya milele, akiwa **Shaheed.**..!

Baada ya kuisha vita, Mtume (saw) na Maswahaba zake walikwenda wakawaangalia Mashuhadaa walipofika katika mwili wa Mus'ab (ra) machozi mengi yaliwatoka...! Walipotaka kumkafini hawakupata ila kijishuka kilikuwa wakikieka kichwani miguu inakua wazi, Na wanapo kiweka miguuni kichwa kinakuwa wazi...! Akasema Rasul (saw): "**Kiwekeni upande wa kichwa na miguu muifunike na majani…!**"

Kisha (saw) akaliangalia shuka lake alilokafiniwa akasema: "**Hakika nimekuona Makkah na ilikuwa hakuna mwenye mavazi mazuri kukuliko, na manukato mazuri kukuliko. Kisha wewe ndiye huyu mwenye nywele tim tim katika shuka**".

**Itaendelea katika UQAB Toleo 14…In Shaa Allah.**

# SWALI / JAWABU:

## Harakati za Urusi na Amerika Nchini Syria
## Hariri ni Mfuasi wa Serikali ya Saudi Arabia





**Swali la Kwanza:** Twajua kuwa Urusi imeingia Syria kupitia makubaliano na Amerika au kupitia maagizo yake kuidumisha serikali hiyo na kuunda mazingira ya suluhisho la kisiasa na upinzani nchini humo. Lakini imeonekana kuwa Amerika inakaribia kuavya juhudi za Urusi za kuleta pamoja serikali na upinzani eneo la Astana na Sochi na mengineo, na inapo hudhuria (mikutano), itafanya hivyo kama mtazamaji tu mithili ya Jordan! Ni upi ufafanuzi wa hili? Shukran.

**Jibu:** Ufafanuzi wa hili unaweza kufupishwa kwa kukusanya maneno mawili: kiburi cha Amerika na ujinga wa Urusi na kuonyesha hilo:

1- Ni kweli kuwa kuingilia kati kwa Urusi kulikuwa kwa ridhaa ya Amerika au maagizo yake kufikia maslahi ya Amerika. Tumefafanua hili siku za nyuma katika taarifa tuliotoa mnamo 11/10/2015, na iliyosema: "… Huu hapa ndio mkakati; Amerika inajidai kuungana na mapinduzi na hivyo kuwa vigumu kuwapiga vita hadharani, na wamesababisha madhara kwa serikali. Kibaraka badala kwa Amerika bado hajapatikana, hivyo basi mchezo wake mchafu ulikuwa ni kwa Urusi kufanya kazi hiyo. Dori yake ni kuisaidia serikali hiyo wazi wazi na kusimama wazi wazi dhidi ya mapinduzi hayo kwa sababu vita dhidi yake vishahalalishwa, na serikali ilikuwa tayari kuiita Urusi kupitia agizo kutoka kwa Amerika. Hicho ndicho kilicho tokea. Urusi imekubali kucheza uovu huu, dori chafu nchini Syria kuihudumia Amerika!" tuliliweka wazi hili katika "Jibu la Swali" tulilotoa mnamo 18/11/2015 kwa anwani: "Maendeleo Mapya katika Uwanja wa Syria", lililo eleza: "…**A-** Uvamizi wa Urusi nchini Syria mnamo 30/9/2015 ulitanguliwa punde tu na mkutano baina ya Obama na Putin mnamo 29/9/2015; mkutano huo ulichukua dakika 90… Mgogoro wa Ukraine ulitawala sehemu ya kwanza ya mkutano huo, huku maraisi hao wawili wakiangazia hali nchini Syria katika sehemu yake iliyo bakia. Matokeo ya mkutano huu moja kwa moja yalionyesha. "Mnamo 30/9/2015 baraza la Urusi (Russian Federation Council) lilipasisha kwa pamoja ombi la Putin la kutumia ndege za kijeshi za Urusi nchini Syria… (Chanzo: Russia Today 30/9/2015)"

**B-** Hata maeneo yaliyo shambuliwa na Urusi nchini Syria mengi yao yalikuwa ni kwa makubaliano na Amerika. Shirika la habari la CNN lilinukuu mnamo 4/10/2015: "Jenerali Andrey Kartapolov, afisa wa kijeshi katika wanajeshi jumla wa jeshi la Urusi, alisema mnamo Jumamosi jioni 3/10/2015 kwamba maeneo yaliyo lengwa na jeshi la anga la Urusi nchini Syria yalikuwa tayari yashatambulishwa kwa Moscow na taasisi ya utoaji maagizo ya kijeshi ya Amerika kama maeneo yanayo ficha magaidi pekee."

Hivyo basi, Amerika iliikaribisha Urusi nchini Syria kusaidia serikali hiyo na kuunda mazingira kwa suluhisho la

*Endelea Uk..13*



Email: info@uqab.or.ke

Kiamerika. Urusi haikuingia Syria kubuni suluhisho kana kwamba ndiyo inayo dhibiti mambo nchini Syria. Lakini ujinga wa Urusi, baada ya maafa iliyo sababisha na kuweza kwake kuzuia kuanguka kwa serikali hiyo, kuliidanganya kufikiri kuwa ingeweza kusimamia suluhisho la kisiasa na kudhani kuwa Amerika haitapinga hili, bali, itakubali maadamu yeye, Urusi, ameongoza dori ya kikatitli nchini Syria kama ilivyo takikana na Amerika na kuilinda serikali kutokana na kuanguka kwake.

2- Kwa msingi wa ufahamu huu wa kimakosa, ikaitisha mikutano maeneo ya Astana na Sochi, na ikaalika makundi nchini humo na kuchora miradi. Na ikaialika Amerika kushiriki na kuwa na dori changamfu ndani yake: "Biskov alisema leo, Jumamosi, kumekuwepo na maendeleo mazuri kuhusiana na suluhu ya Syria katika muda wa hivi karibuni, "Lakini inahitaji juhudi za pamoja kuyafikisha katika hatua mpya yenye thamani, yote haya yahitajia Urusi kuamiliana na Amerika katika njia moja au nyengine…" (Chanzo: Orient News 4/11/2017). Urusi ilikuwa inatarajia kufanya mkutano baina ya raisi Putin na raisi wa Amerika Trump nchini Vietnam katika kongamano la APEC mnamo 10/11/2017, na imekuwa ikikariri na kuitisha mkutano wazi wazi baina ya maraisi hao wawili hata wakati wa kongamano hilo katika hali inayo ashiria haja ya Urusi kushirikiana na Amerika katika mahusiano baina ya nchi hizo juu ya Syria, lakini Amerika haikujibu na ikakubali tu kutoa taarifa ya pamoja ya maraisi hao wawili kana kwamba mkutano huo tayari umefanyika ingawa si kwa kiwango cha kimkutano, ilikuwa ni taarifa iliyo tayarishwa na wajuzi kutoka pande zote mbili na hatimaye kupeana mikono kwa maraisi hao wawili. Huu ni mfano wa Urusi kuiomba Amerika, inayo dhihirisha kutiwa aibu.

3- Urusi wakati huo huo inajua kuwa haiwezi kufanya hivyo bila ya Amerika, na inaendelea kuiomba ikitaraji kupata majibu; aina ya idhilali inayo anza kujitokeza, kama ilivyo tajwa juu kwa kutaka kwake mkutano baina ya Putin na Trump.

Na kwa sababu Urusi inakimbilia kupata suluhisho nchini Syria, raisi wake, Putin, alimualika mhalifu Bashar kufanya naye mkutano eneo la Sochi mnamo 20/11/2017, na kisha kuwasiliana na Trump mnamo 21/11/2017, akimwambia namna ya mazungumzo kati yake na Bashar yalivyo kwenda: "Raisi wa Urusi Vladimir Putin alimpigia simu leo,Jumanne, mwenzake wa Amerika Donald Trump, iliyo angazia juu ya mgororo nchini Syria na matokeo ya mkutano wake na Bashar al-Assad. (Chanzo: Russia Today 21/11/2017)

Hivyo basi, Urusi inapapatiko la kutaka kuharakisha suluhisho la mgogoro wa Syria, na kuota mchana kama kawaida yake kuwa yeye ni dola kuu inayo chukua nafasi sako kwa bako na Amerika katika kutatua mgogoro wa syria, kwa hivyo tunaiona kuwa na hamu kupata suluhisho la kisiasa leo kwa kuwa ndilo litakalo ipatia hadhi katika kuondoka kwake. Suluhisho hili la kisiasa litasitisha kudhaifika kwake hususan katika uchumi kama natija ya kushiriki kwake kijeshi. Kutokana na yote haya, ikachukua hatua ya kufanya mikutano iliyotoa sura ya kuwa yeye ni kiongozi anayeongoza juhudi za kupatikana suluhu nchini Syria; hivyo basi, ikamshurutisha Bashar, kisha Erdogan na Rouhani, na kisha kupanga kuwaita wale wanaojulikana kama wawakilishi wa "matabaka yote ya Syria" kutafuta suluhu ya mgogoro huo. Urusi inainyenyekea Amerika kushiriki mchakato huu ili kufikia suluhisho la haraka, imetangaza nia yake ya kuondoa baadhi ya wanajeshi wake: "Huenda ikachangia pakubwa kupunguza idadi ya jeshi la Urusi nchini Syria "katika athari inayohisika wazi wazi" na huenda ikaanza kabla ya mwisho wa mwaka huu," akasema Valery Gerasimov, mkuu wa jeshi la Urusi, mnamo Alhamisi… (Chanzo: euronews 23/11/2017). Lakini, Amerika inakwenda kwa mwendo wa kinyonga katika kujibu maombi ya Urusi.

4- Huu ndio mchezo wa Amerika pamoja na Urusi kuhusiana na Syria, yaani, kuitenga na kutelekeza matakwa yake na kutosimama nayo isipokuwa katika kadhia chache na aghalabu ni kwa kupitia wafuasi wake, jambo linaloonyesha kuwa juhudi za Urusi kuongoza suluhisho la kisiasa nchini Syria zitasambaratika kutokana na Urusi kuanguka ndani ya shimo la Amerika nchini Syria. Kile ambacho Amerika inakinyamazia kimya na kukishajiisha ni kuendelea kuitumia Urusi kama moja ya vifaa vya utawala wa Amerika nchini Syria dhidi ya mapinduzi na athari ya Uislamu ndani yake; Urusi haina dori yoyote ya kuongoza kutatua mgogoro nchini Syria licha ya kuoneka mandhari ya mikutano na makongamano mingi na kupokelewa kwake jijini Moscow na Sochi…

Na kabla ya njia ya Urusi na Amerika kuwa wazi, mipango yote ya Urusi kwa ajili ya suluhisho nchini Syria itasalia kuwa dhaifu ikisubiri kushiriki kwa Amerika. Pindi chembe chembe za suluhisho hilo zitakapo komaa nchini Syria, Amerika inatarajiwa kusonga mbele kupitia Umoja wa Mataifa au kupitia washirika wake wa eneo kulazimisha suluhisho nchini Syria.

5- Hivi ndivyo inavyo jitokeza kwa harakati za Urusi na Amerika nchini Syria, ambazo zaweza kutunguliwa, Allah akitaka, ikiwa makundi ya wapiganaji yatafuata njia iliyo nyoka na kuvunja mafungamano yao na vibaraka wa Amerika wa eneo, hususan Uturuki na Saudi Arabia, na kisha kusimama kidete mbele ya serikali kwa ikhlasi na kushirikiana na wenye ikhlasi miongoni mwa Umma, kwa kushikana na Kamba ya Allah. Hapo ndipo Syria, itakapo kuwa izara kwa Amerika na Urusi, na itakapo kuwa ni yenye kuwavunja migongo yao wote wawili na kutoka huku wakiwa wameshindwa, wakikimbia pasi na kujali chochote chengine nyuma yao. Hili si gumu kwa Alllah kulitimiza.

================

Endelea Uk..14

**Swali la pili:** Hariri amerudi tena kutoka katika hali ya kujiuzulu kwake na wizara ikakutana chini ya uenyekiti wake mnamo 5/12/2017. Kisha akasema kuwa wizara hiyo imekubali "kutoingilia kati kadhia (nje ya Lebanon)" kufuatia vitendo vya Hariri, fazaa na migongano ilijitokeza: Baada ya miaka mitano ya kukosekana raisi nchini Lebanon, Hariri alikwenda kwa Aoun mnamo 20/10/2016 na kukubaliana naye juu ya uraisi na serikali, akijua kwamba Aoun na Hezbollah ni kundi moja na kwamba Hezbollah ndiye mhusika mkuu. Mnamo 04/11/2017, Hariri alitangaza kujiuzulu kwake nchini Saudi Arabia na kumwaga hasira zake kwa Hezbollah. Ulibatilisha kujiuzulu kwake huku na kuendelea na serikali, ikiwemo Hezbollah! Ni upi ufafanuzi wa fazaa hii na mgongano huu? Na je, uko muelekeo wa kupunguza ushawishi wa Iran na chama chake? Je, watarajia uvamizi kutoka kwa dola ya Kiyahudi kwa Lebanon au kwa Hezbollah, kwa kupatiliza fursa ya dhurufu zilizoko kwa sasa? Jazakallah.

**Jibu:** Ili kuweka wazi jibu hili, ni muhimu kutaja uhalisia wa uhusiano kati ya familia ya Hariri na Saudi Arabia: Hariri ni mfuasi wa Saudi Arabia. Ikiwa mtawala wa Saudia ni mtiifu kwa Uingereza basi hili pia litatarajiwa kwa Hariri, katika miondoko yake, katika sera zake nchini Lebanon na hali kadhalika ikiwa huyo ni mtiifu kwa Amerika. Kwa msingi huu, twaweza kujibu yafuatayo:

1- Muhula wa aliyekuwa raisi wa Lebanon Michel Suleiman ulimalizika mnamo Mei 2014, na mtawala nchini Saudi Arabia alikuwa Mfalme Abdullah bin Abdul Aziz, na kwa sababu Abdullah alikuwa mtiifu kwa Uingereza na kwa kuwa Hezbollah ilikuwa imejitolea kuhakikisha inamfanya Aoun kuwa raisi, na inajulikana kuwa Hezbollah na Aoun wanapewa usaidizi na Iran kibaraka wa Amerika, Mfalme Abdullah hakukubaliana na chaguo la Aoun kuwa raisi wa Lebanon, na hivyo basi kumuagiza Saad Hariri kupinga ugombezi wa uraisi wa Aoun. Saad Hariri sera yake aliichukua kutoka kwa sera ya Saudia, yaani sera ya Abdullah na hivyo basi nafasi kiti cha uraisi wa Jamhuri ya Lebanon imekuwa wazi kwa muda wa zaidi ya miaka miwili na nusu tangu kumalizika kwa muhula wa Michel Suleiman mnamo Mei 2014 mpaka mchana wa Jumatatu ambapo bunge la Lebanon lilikutana na kuchaguliwa kwa Aoun kama raisi wa Jamhuri hiyo na hayo yalikuwa mnamo 31/10/2016.

2- Kilicho saidia ni mabadiliko ya utawala nchini Saudi Arabia. Mfalme Abdullah alifariki mnamo Januari 23/1/2015, na kakake, Salman, kuchukua uongozi kutoka kwake. Kama ilivyo maarufu, yeye ni kibaraka wa Amerika. Mfalme huyu alianza kwa kuwakata mabawa watoto wa Abdullah ambao ni vibaraka wa Uingereza na waliokuwa wafuasi wake mpaka alivyoweza kuyaimarisha mazingira ya utawala wake. Baada ya mambo kutulia, na kwa sababu Amerika ilitaka kumakinisha hali nchini Lebanon kwa njia ya kivyake yeye kupitia kumchagua Aoun kama raisi wa Jamhuri hiyo, Amerika ilimuagiza Salman kumuagiza Hariri kutopinga hili! Hiyo ndio sababu Saad Hariri alikwenda kwa Aoun na kukubaliana naye na kumteua kama mgombezi wa uraisi wa nchi hiyo. Kwa maana nyengine ni kuwa, upinzani ulioongozwa na Saad Hariri katika enzi za Abdullah umemalizika katika enzi ya Salman! (Raisi Saad Hariri aliwasili kutoka makao yake (Bait Al-Wasat) na kumteua mbunge Michel Aoun kuwa mgombezi wa uraisi wa Jamhuri hiyo mbele ya wanachama wa chama chake, wakiongozwa na Raisi Fuad Siniora na mbunge Bahia Hariri. Kisha akatoa hotuba ambapo alisema: "Kwa msingi wa nukta za makubaliano tulizofikia, natangaza mbele yenu leo uamuzi wangu wa kuunga mkono kuchaguliwa kwa Jenerali Michel Aoun kuwa Raisi wa Jamhuri hii"… Chanzo: An-Nahar 20/10/2016).

Baada ya hayo, bunge la nchi hiyo lilikutana mnamo 31/10/2016 na Aoun akachaguliwa Raisi wa Jamhuri…" Uungaji mkono huu wa kiongozi wa chama cha Al-Mustaqbal, Saad Hariri, uliharakisha uchaguzi wa uraisi baada ya kiti hicho kukaa wazi kwa muda wa miaka miwili na miezi mitano tangu kumalizika kwa muhula wa aliyekuwa Raisi wa Lebanon Michel Suleiman mnamo Mei 2014… Chanzo: al-Arabiya 31/10/2017), na hivyo basi ziara ya Aoun nchini Saudi Arabia ilikuwa ni kuonyesha shukrani zake! Kama ilivyo wazi katika maelezo ya juu, Hariri ni mfuasi wa mtawala wa Saudi Arabia, kwa hivyo atapinga au kukubali kile atakacho onyeshwa na mtawala wa Saudi Arabia.

3- Baada ya Trump kuchukua uongozi wa Amerika, alizuru Saudi Arabia mnamo 20/05/2017 na kutoa taarifa kali kuhusu Iran na Hezbollah. Alilenga kutoa taarifa hizo kali kabla ya kongamano la takriban viongozi 50 walegevu wa Waislamu kuziba macho juu ya kadhia ya Waislamu wa Palestina na kuwafanya waangazie juu ya Iran, ambapo ilikuwa ni utangulizi wa kile alichokuwa anakipanga, kuitambua Jerusalem kuwa mji mkuu wa Mayahudi. Ilikuwa wazi katika taarifa hizo katika kukokotezwa ukali wake. Bila shaka, Saudi Arabia na nchi nyenginezo miongoni mwa wafuasi wake zimetabanni muelekeo huu. Na kwa kuwa dori kuu ya Iran katika eneo hilo imetawaliwa na vitendo vya Hezbollah nchini Lebanon na kuingilia kati kwake nchini Syria, Saudi Arabia ilimuagiza Hariri kuwa mpinzani wa Hezbollah na Iran. Hivyo walimuita nchini Saudi Arabia na kumuagiza kujiuzulu huko na kutoa sababu zake kupitia taarifa kali dhidi ya Iran na Hezbollah. Kwa hayo, Hariri aliletwa nchini Saudi Arabia na kutoa taarifa yake kali, na kutangaza kujiuzulu kwake nchini Saudi Arabia mnamo 04/11/2017M.

4- Amerika inafahamu kuwa taarifa zake dhidi ya Iran na Hezbollah hazimaanishi mzozo kati ya Iran na chama chake, bali ni mkokotezo wa kupatiliza fursa ya hofu ya wakaazi wa Ghuba; ndilo lililotakikana kwa Saudi Arabia na Hariri kutuma ujumbe, lakini si

*Endelea Uk..15*

kufuata barabara hii mpaka mwisho. Kwa maana nyengine ni kuwa, Amerika haitaki kumaliza uwepo wa chama chake, bali kutuma tu ujumbe uliotathminiwa pasi na kuchochea hali nchini Lebanon. Hii ndio sababu iliiagiza Saudia kuleta utulivu, yaani kumfanya Hariri kupunguza sauti yake. katika tovuti ya An-Nashra mnamo 04/12/2017, ilieleza: "…Mfalme Mtarajiwa wa Saudia, Muhammad bin Salman, hakuchukua hatua isipokuwa baada ya maelekezo kutoka ikulu ya White House, na baada ya ziara ya nne ya mshauri mkuu wa Raisi wa Amerika mkwewe Jared Kushner katika Mashariki ya Kati tangu Raisi Donald Trump kuchukua mamlaka, ziara hii iliwekwa mbali machoni mwa vyombo vya habari. Kushner na ujumbe wake nchini Saudia ulikaa siku nne ikihusisha ziara za mara kwa mara nchini Misri na Jordan na "Israel". Takriban wiki mbili baada ya kuondoka Kushner, migogoro nchini Lebanon na ukamataji nchini Saudi Arabia ikalipuka. Wakati ambapo migogoro mibaya ya kisiasa ilipo ishambulia Lebanon, dalili ziliibuka kuwa kuna maelewano kati ya ikulu ya White House na Mfalme Mtarajiwa wa Saudia juu ya Lebanon nayo ni kuishinikiza Hezbollah kufanya marekebisho ya ukubwa wa eneo lake baada ukubwa wa eneo lake kuongezaka. Chini ya anwani hii, Mfalme huyo Mtarajiwa wa Saudia alianzisha mashambulizi yake kwa serikali ya Lebanon kupitia Waziri Mkuu wake, Saad Hariri, na hivyo basi kuvuruga makubaliano ya kati na kati yaliyo fanyika kwa kuwasili kwa Jenerali Michel Aoun katika kasri la Baabda. Lakini mbinu ya Saudia ilikuwa ya vurugu iliyokosa hekima ya kidiplomasia, iliyo hatarisha utulivu wa kindani nchini Lebanon. Huku taasisi za Kiamerika zikiendelea kukariri kuwa shinikizo hili linalo lengwa Hezbollah linadhibitiwa na mipaka maalumu ambayo hakuna anayeruhusiwa kuivuka ili kuchunga kuharibika kwa hali nchini humo. Huku mambo yakizorota, taasisi za Kiimerika zilichukua hatua kwa msingi kuwa utulivu wa Lebanon uko katika hatari ya kuporomoka… (Chanzo: Tovuti ya An-Nashra: 04/12/2017)

Hivyo basi, Hariri akaanza kulainisha sauti yake kwa maagizo ya Saudi Arabia. Ili kuokoa uso wake, Saudi Arabia ilimpokea Raisi wa Ufaransa na kufanya mazungumzo naye na kukutana na Hariri. Kisha Hariri akasafiri hadi Ufaransa na kisha Misri na kuunda mazingira kana kwamba anawashauri ili kuchukua msimamo unaostahili ingawa mandhari yalionekana wazi nchini Saudi Arabia kabla ya kuondoka kwake, ambayo ni kulainisha sauti yake na kutojiuzulu. Haya ndio yaliyotokea; aliregea nchini Lebanon mnamo 22/11/2017 na kisha kupunguza sauti yake kwa kiwango kikubwa dhidi ya Hezbollah, na kusema kuwa Hezbollah haitumii silaha zake nyumbani, kana kwamba anajidanganya mwenyewe kabla ya kuwadanganya wengine, na kusahau kuwa Hezbollah hutumia silaha zao ndani ya Lebanon zaidi ya mara moja mpaka wakati alipo tangaza kusitisha kujiuzulu kwake na kuitisha mkutano wa baraza la mawaziri chini ya uenyekiti wake mnamo 05/12/2017. Alisema katika taarifa yake (… kwamba hali ya utilivu imeregea baada ya uidhinishaji wa wanachama wote wa serikali wa kujiweka mbali na kadhia za nchi za kiarabu) alisema haya, huku wanamgambo wa Hezbollah wanapigana nchini Syria usiku na mchana!

6- Kwa mukhtasari, Hariri ni mfuasi wa utawala wa Saudi Arabia na sera yake kama mtawala inategemea Saudi Arabia, na utiifu wake unaashiriwa kwa maagizo yake kwake. Hili sio siri, na ni bure kuwapotosha watu kulihusu!

Kwa hivyo kutakuwepo na hatua ya kupunguza ushawishi wa Iran na chama chake, na hili lawezekana, lakini linatarajiwa kufanyika baada kufikia suluhusho nchini Syria kwa kiwango kinacho takikana na Amerika, kisha ikiwa dori za Iran na Hezbollah zitakamilika, huenda ikajiondoa nchini Syria na kupunguza dori ya kijeshi ya Iran na chama chake. Kwa taarifa yako, Hezbollah ni tagaa la serikali ya Iran kama alivyo Hariri tagaa kwa serikali ya Saudi Arabia. Hivyo basi, inatarajiwa kuwa ikiwa kadhia ya Syria itamalizika kwa mipangilio maalumu ya kujiondoa kwa Iran, mipangilio maalumu mengine itafuata kwa chama chake nchini Lebanon.

Je, kuna uvamizi wowote unaotarajiwa wa dola ya Kiyahudi kwa Lebanon na Hezbollah? Hii itategemea mipangilio ya suluhisho nchini Syria, ambayo inategemea dhurufu zilizoko kwa sasa na dhurufu mpya.

**21 Rabii' Al Awwal 1439 H**
**9/12/2017 M**

بسم الله الرحمن الرحيم

**Hizb ut Tahrir Kenya inafuraha kuwatangazia wafuatiliaji na wageni wake wanaozuru Tovuti na Mitandao ya Kijamii yake kuwa kufikia 1 Februari 2018 itakuwa MWAKA 1 tangu kuzinduliwa kwa Jarida la UQAB la aina yake. Jarida la kila Mwezi ambalo linatoa uchanganuzi na suluhisho za kimfumo kwa kina. Sasa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt), tunaadhimisha Mwaka huo kwa kuzindua RASMI TOVUTI YA JARIDA LA UQAB pamoja na MITANDAO YAKE RASMI YA KIJAMII**

**LINK RASMI ZA JARIDA LA UQAB:**

**Tovuti: uqab.or.ke**

**FACEBOOK: UQAB-Magazine-1911964012162253**

**Twitter: uqab_htk**

**Instagram: uqab_htk**

**Tafadhali LIKE, SHARE, RETWEET na FOLLOW kupitia Link hizo hapo Juu**

**Kwa Matoleo Yajayo…**

